2. Baada ya Unyakuo…
Barua ya upendo kutoka Mwenyezi Mungu kwa wale waliobaki

(Love Letter from God for the Left Behind… After the Rapture in Swahili)

Oktoba 7th, 2014

Nakuita wewe, nikikupatia faraja kwa moyo wako – sijakuwacha na sitawahi kukuwacha ama kukusaliti wewe. Najua vizuri sana uchungu unayohisi. Wakati nyingine unahisi kusalitiwa. Maswali yako yote unayouliza mbona, wapi na kwa nini bado niko hapa, mbona niliwachwa nyuma na nitafanya nini sasa?

Lazima upinge majaribio ya kurudi tena kwa maneno ya dunia na kuchukua faida kwa nafasi mpya za kazi na cheo, kwa ajili ya uwezo wa kujaza hizi nafasi za kazi, biashara, na maneno yote yanayohusu pesa kwa dunia.

La hasha, hata kwa uchungu unayohisi na pia kuchanganyikiwa, wachana na haya maneno ya pesa, mjitoe kwa hii dunia isiyoimara na mnitafute mimi Yesu na moyo yenu yote kama haujawahi kwa maisha yako, njoo kwangu Yesu ukitubu dhambi na ukiwa umebadilika moyo na nitakusaidia, kuwa pia nitapuuza hofu na nitakukaribisha kwangu tena kwa mikono wazi.

Haujapotea, kwa masiku yanayowadia utapata kuona kweli kwa namna kubwa vile ninavyokupenda. Ujue mama akisaliti na kuwacha mtoto, Mimi siwezi kukusailiti ama kukuwacha, niko hapa milele kukuokoa – bado wewe ni mtoto wangu na mwenye thamani kubwa kwangu. Wewe ni hazina wangu na niko nawe hata sahi.

Swali linalokusumbua akilini kwa sasa, ni mbona Mungu wangu, mbona? Kwa nini niliwachwa nyuma? Mtoto wangu, haukufaa kuwachwa nyuma kwa unyakuo, ilikuwa huruma yangu Yesu wako kwa watoto wangu wote, kanisa yangu, mwili wangu, bibi harusi wangu. Ulikuwa unafaa kunyakuliwa, ili ningeweza kukuzuia kuishi na kuona wakati wa kutishia kupindukia kwa mateso duniani, haijawahi kuonekana na haitawahi kuonekana milele.

Ulianza vizuri, walakini wakati iliyopita ulianza kuingilia maneno ya dunia kuzidi, ingawa bado ulikuwepo Mkristu kwa jina langu Yesu, ulianza kupotea kuzidi kwa maneno ya dunia, na mengi yalikuzingua na kukuzubaisha wakati uliopita, wakati ambayo tuliyokuwa tunashirikiana pamoja ilididimia sana.

Ulijua ya kwamba ulikuwa unaingilia maneno ya dunia kuzidi na ilikuwa inazuia imani yako na uliwacha kuniongelesha, hiyo na uhusiano mapya na watu na kuongezea, jinsi mpya uliyokuwa nayo kwa fikira ilifanya uanze kuhukumu roho zilizokuzunguka na zilizokaribu nawe. Ulianza kuwadharau na vile vitu walivyopenda, kuzidi, ulidharau furaha zao zile walizokuwa nazo kuhusu kurudi kwangu, Yesu wako, kwa dunia.

Na wakati nilipofika, kile tu ungefanya ni kusimama kwa hofu na aibu, kwasababu kile kitu ulichofaa kuamini, kilikuwa kimetendeka mbele yako, kwasababu haukuamini na haukuwa mwangalifu na haukuomba, kwamba nilikuja kama mwizi katika usiku na haukuwa tayari. Kwa hivyo singeweza kukuchukua.

Unaniuliza sahi, nifanye nini sasa? Keti karibu nami kama haujwahi maishani mwako. Omba ili upate neema yangu kwa moyo na akili yako, omba jina langu libaki kwa ulimi wako, lazima unishikilie kwa nguvu nguo yangu na usiwahi, hata kwa nukta moja, kuniwacha tena. Endeleza tabia ya kunishukuru kwa kila wakati na kwa kila pahali.

Kuwa na mimi kwa kila wakati akilini mwako. Lazima ushinde ukiomba ili niweze kukupa hii uwezo, na bila shaka nitakupa hii uwezo. Tayrai niko nawe, lakini inakubidi uweze kunihisi karibu nawe, ongea na mimi, ongea na mimi kama rafiki wako mpendwa uliomwamini wa kipekee. Napenda sana kujua fikira zako zote na vile unavyohisi kwa kila wakati, bora ujitahidi kuwa mnyenyekevu, na kuwa mdogo sana kwa macho yako. Milele na milele nitakuwa rafiki yako wa kipekee uliyemwamini na kumpatia siri zako zote. Hunivutia sana, roho ndogo zilizokuwa kama za watoto wadogo.

Mimi hukaa karibu na hizi roho kushinda ngozi zao na ujue nitakuwa na wewe. Najua ya kwamba bado umechanganyikiwa sana na ujue dunia mzima imechanganyikiwa sana pia. Walakini najua, tayari umeanza kuhisi amani na utulivu usiyoweza kuelewa ama kueleza.

Nitaendelea kukupa hii zawadi ya amani na utulivu na utajipata ukiwa na uwezo wa kufikiria kwa uwazi usioeleweka. Usijali kuhusu mahitaji yako, kwa vile unavyoona, nimkupa kile unachohitaji kwa kila njia, watu wataendelea kukupa kila kitu unachohitaji bila wewe kuyatarajia na utaanza kuhisi kwa haraka, kweli uzuri wa amani, hata kwa jinsi dunia ilivyochanganyikiwa kwa sasa.
Hakuna kitu chochote kwa dunia iliyonishinda kudhibiti na hakuna kitu chochote inachoruhusiwa bila kupenda kwangu. Nishatayrisha mahitaji yako yote mbele ya wakati utakaowadia.

Usiwe na wasiwasi yoyote, kitu cha pekee ni kuweka moyo na macho yako kwangu Yesu, wewe ni thamani wangu, mtoto wangu yule ambaye sitaruhusu mtu yeyote ama kitu chochote kikudhuru. Nimetuma malaika wangu wakukinge na wakuchunge mchana na usiku. Utapata mahitaji yote na zaidi ya hayo utajua upendo wangu na ukweli uaminifu wangu, kuwa nitawajaza watoto wangu wote na mahitaji yao kuzidi.

Utaanza kupatana na wengine kama wewe waliotubu dhambi na wale waliovunjwa moyo na roho, ambao watakaorejeshwa kwa unyenyekevu mwingi na moyo zao zikuwe zangu pekee mbinguni kwa Baba yangu, Mungu wetu wa pekee. Nitakusanya watoto wangu tena, kama vile mama na watoto wake, na nitawapa ushindi wa huu wakati wa majaribio mengi. Watametameta kama nyota za mbinguni. Watatawala kando yangu mbinguni kwa vile wamevumilia na wamekuwa watukufu kwa wakati wa majaribio na dhiki.